

Ufafanuzi Linganishi wa Kimofolojia katika Mizizi ya Vitenzi vya Kiswahili vyenye Asili ya Kiarabu na vile vya Kiswahili Asilia

Johari Hakimu
Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe

jhakimu@gmail.com

Ikisiri

Makala hii inahusu ufafanuzi linganishi wa kimofolojia katika mizizi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu na vile vya Kiswahili asilia. Lengo la ulinganishi huu ni kuweka wazi kufanana na kutofautiana kwa mizizi hiyo ili kuonesha mipaka iliyopo katika uchanganuzi wa vitenzi hivyo. Ulinganishaji huo umefanyika kwa kutumia data ya vitenzi iliyopatikana katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili* ya BAKITA (2017). Pia, mifano na ufafanuzi uliotolewa na wataalamu mbalimbali kuhusu mizizi ya maneno ya Kiswahili imesaidia kuonesha ukweli kuhusu mizizi ya vitenzi vya Kiswahili asilia. Data hiyo imeshughulikiwa kwa kuzingatia kiunzi cha Nadharia ya Mofolojia Leksika, ambapo mihimili miwili ya nadharia hiyo imehusishwa. Mihimili iliyohusishwa ni kanuni ya kufuta mabano na kanuni ya mzunguko kamili. Kwa hiyo, ufanano na utofauti wa vitenzi hivyo umedhihirika. Katika mazingira kadhaa, mizizi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vimefanana na vya Kiswahili asilia kutokana na utegemezi wa mizizi yake na katika baadhi ya miundo ya mizizi. Pia, vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vimetofautiana na vile vya Kiswahili asilia kutokana na vitenzi hivyo kuwa na mizizi huru michache na baadhi ya miundo ya mizizi hiyo kutofautiana.

Dhana za Msingi: Mofolojia, vitenzi vya Kiswahili asilia, Kiarabu

Utangulizi

Vitenzi vya Kiswahili vinajumuisha vitenzi vya Kiswahili asilia na vile vilivyokopwa kutoka katika lugha zingine. Makala hii imeshughulikia ufafanuzi linganishi wa mizizi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu na vile vya Kiswahili asilia. Vitenzi vya Kiswahili asilia na vyenye asili ya Kiarabu vina namna vinavyofanana na kutofautiana katika uchanganuzi wake kimofolojia. Kwa hiyo, makala hii inalenga kuonesha mipaka iliyopo baina ya uchanganuzi wa mizizi ya vitenzi hivyo. Hii itawasaidia wajifunzaji na wafundishaji wa mofolojia kushughulikia mizizi ya vitenzi vya Kiswahili kwa kujua tofauti zilizopo baina yake. Mizizi ya vitenzi vya Kiswahili katika ujumla wake imekuwa ikishughulikiwa na wataalamu mbalimbali bila kuweka tofauti zake wazi. Wataalamu hao ni pamoja na Hurskainen (1992), Ud Deen (2005), Mgullu (2012), Wesana-Chomi (2013), na Mugaya (2019).

Dhana ya mzizi wa neno imefasiliwa kwa ujumla na Massamba (2004:61) kuwa ni sehemu ya neno ambayo ndiyo kiini cha maana na ambayo haiwezi kuchanganuliwa zaidi bila kupoteza utambulisho wake. Mzizi wa maneno ya Kiswahili umeshughulikiwa na Mgullu (2012:103 - 104) ambapo ameufafanua mzizi wa maneno ya Kiswahili kwa ujumla huku akionesha aina za mizizi ya maneno. Pia, pamoja na kwamba Mgullu (2012:182 - 212) anafafanua na kuonesha uchanganuzi wa vitenzi vya Kiswahili kwa ujumla yaani vya Kiswahili asili na vile vyenye asili ya Kiarabu, haoneshi namna uchanganuzi wa vitenzi hivyo kimofolojia unavyofanana na kutofautiana. Vilevile, kama Mgullu, Wesana-Chomi (2013:22) ameufafanua mzizi wa maneno kwa ujumla bila kuangalia namna unavyojitokeza katika vitenzi vya Kiswahili kwa ujumla. Pia, Mugaya (2019:74 - 79) amielezea dhana ya mzizi, aina za mzizi, sifa za mzizi na ubainishaji wa mzizi. Katika hayo,

haikuoneshwa wazi ni kwa namna gani uchanganuzi wa mzizi wa vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu unavyafanana na kutofautiana na wa vile vya Kiswahili asilia.

Nadharia ya Utafiti

Uchanganuzi wa muundo wa mzizi umezingatia kiunzi cha Nadharia ya Mofolojia Leksika cha Kiparsky (1982). Nadharia hiyo ina mihimili mbalimbali ambayo ni pamoja na kanuni ya ngazi leksika, kanuni ya mzunguko kamili, kanuni ya kufuta mabano, kanuni ya ufinyu wa sifa, na kanuni ya kuhifadhi muundo (Katamba, 1993; Gichuru, 2010; Buberwa, 2015). Kutokana na mihimili hiyo, makala hii imetumia mihimili miwili ambayo ni kanuni ya kufuta mabano na ile ya mzunguko kamili katika uchanganuzi. Kwa hiyo, kanuni ya kufuta mabano imetumika ili kuonesha mpaka na nafasi ya kila kiambishi katika maneno. Mabano yanayotenganisha viambishi vinavyounda neno yakifutwa, umbo la neno zima hudhahirika. Kanuni hii inahusiana na msingi mmojawapo wa nadharia hii kwamba ni lazima kila kiambishi kioneshwe ni kwenye nafasi gani ya neno kinaweza kuambikwa, kiwe kinatokea kabla au baada ya mzizi pamoja na sifa yake (Massamba, 2011). Hata hivyo, katika kuonesha mipaka ya viambishi katika vitenzi, kimetumika kistari (-) badala ya mabano ([]) katika makala hii ili kutenganisha mzizi na viambishi vingine kwa sababu data imewasilishwa kwenye majedwali katika baadhi ya maeneo.

Vilevile, mhimili wa kanuni ya mzunguko unaohusiana na msingi wa nadharia hii unaohusu upangiliaji wa vipashio vya kimofolojia kidarajia (Allen, 1978; Pesetsky, 1979; Kiparsky, 1982; 1983; Pulleyblank, 1986, kama wanavyorejelewa na Katamba, 1993), umetumika ili kuonesha mabadiliko kadhaa ya kifonolojia na kimofolojia katika ubainishaji wa

mizizi ya vitenzi. Hii ni kwa sababu, kuna uhusiano wa karibu kati ya kanuni za kimofolojia na zile za kifonolojia katika kila darajia ya uundaji wa neno (Kiparsky, 1982; Katamba, 1993; Hakimu, 2020). Kanuni hizo ni kanuni za kimzunguko zinazojirudia katika baadhi ya mabadiliko ya kimofolojia na kifonolojia katika darajia maalumu ya uundaji wa maneno. Darajia hiyo inaweza kuwa katika kiwango cha mpaka wa unyambuzi na uambatizi, unyambuzi na uambatanishaji pamoja na uambatizi (Kiparsky, 1982). Kwa hiyo, mhimili huu umesaidia kubainisha namna baadhi ya mizizi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu inavyojitokeza. Ubainishaji wa mizizi hiyo (ambao ni tokeo la kimofolojia) katika mpaka wa unyambuzi unategemea mabadiliko ya sauti (ambalo ni tokeo la kifonolojia).

Methodolojia

Data iliyotumika katika makala ilikusanywa kwa njia ya upitiaji wa nyaraka katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili* ya BAKITA (2017). Katika kamusi hiyo, vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu na vile vya Kiswahili asilia vilikusanywa. Vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vilikusanywa vyote ili kupata mwanya mpana wa kuona utokeaji wake. Hii ilichochea na tabia ya vitenzi hivyo kutokuwa na irabu maalumu mwishoni mwa mashina yake tofauti na vile vya Kiswahili asilia vinavyoishia na irabu {-a}. Kwa ujumla, vitenzi vilivyoingizwa katika kamusi na kutolewa maana (vidahizo) vilikusanywa pamoja na vinyambuo vyake vya kauli mbalimbali za vitenzi. Vinyambuo hivyo ndivyo vilivyochanganuliwa ili kulinganisha mizizi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu na vile vya Kiswahili asilia. Vidahizo vilivyokusanywa vilibaki kama virejewa kwa ajili ya kuona vitenzi vilivyokuwa kabla ya kuambikwa viambishi mbalimbali. Hii ilisaidia kufuatilia mabadiliko yanayojitokeza katika mizizi

ya vitenzi baada ya kuambikwa viambishi mbalimbali kwa kurejea umbo lake la awali (kidahizo).

Mchakato wa ukusanyaji wa vitenzi ulizingatia kategoria ya neno, irabu zake za mwishoni na etimolojia za maneno. Kwa kuzingatia kategoria ya neno, vitenzi vilitambuliwa kwa sababu *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (KKK) imeonesha kategoria za vidahizo vyote vilivyoingizwa katika kamusi hiyo. Pia, uzingatiaji wa irabu za mwishoni mwa vitenzi ulisaidia kwa sababu, vitenzi vingi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu huishia na irabu {-e, -i na -u} (Polome, 1967) kama *samehe*, *fadhili* na *sahau*. Vitenzi vichache vyenye asili ya Kiarabu na vyote vya Kiswahili asilia huishia na {-a} kama *rejea*, *soma* na *jenga*. Kwa hiyo, kutokana na irabu hizo ilikuwa rahisi kuvibaini na kuvikusanya. Sambamba na hayo, etimolojia ya kitenzi ilizingatiwa kwa sababu KKK ina maneno mengine ya Kiswahili yenye asili za kigeni kama Kiingereza yanayoishia na baadhi ya irabu hizo. Hivyo, uzingatiaji wa etimolojia ulisaidia kujua asili ya vitenzi kwa usahihi zaidi pamoja na asili ya vile vinavyoishia na irabu {-a}. Hii ni kwa sababu, vitenzi hivyo (vyenye asili ya Kiarabu) vinavyoishia na irabu {-a} vimefanana na vile vya Kiswahili asilia kutokana na uishiaji wa irabu hiyohiyo. Mbali na data iliyokusanywa kutoka KKK, mifano iliyotumiwa na ufafanuzi wa wataalamu mbalimbali kama Ud Deen (2005), Mgullu (2012), Wesana-Chomi (2013) na Mdee (2016) imesaidia kubaini mizizi ya vitenzi vya Kiswahili asilia ilivyo.

Vilevile, data ilichanganuliwa kwa kuzingatia kanuni ya kufuta mabano na mzunguko kamili za Nadharia ya Mofolojia Leksika. Kama ilivyoielezwa katika utangulizi, kanuni ya kufuta mabano ilitumika ili kuonesha mpaka na

nafasi ya kila kiambishi katika maneno. Pia, kanuni ya mzunguko kamili inayohusiana na msingi (wa nadharia hii) unaohusu upangiliaji wa vipashio vya kimofolojia kidarajia (Allen, 1978; Pesetsky, 1979; Kiparsky, 1982; 1983; Pulleyblank, 1986, kama wanavyorejelewa na Katamba, 1993) imetumika. Upangiliaji wa vipashio katika darajia hizo huonesha athari za mwingiliano wa kanuni za fonolojia na mofolojia kutokana na uambikaji wa viambishi mbalimbali katika mizizi. Kwa hiyo, ukomo wa uchanganuzi wa data ulitegemea utoshelevu wake kwa vitenzi vyote vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu na vile vya Kiswahili asilia.

Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yamegawanywa katika vipengele mbalimbali. Navyo ni mzizi wa kitenzi, aina za mzizi, muundo wa mzizi wa vitenzi vya Kiswahili asilia na vile vyenye asili ya Kiarabu.

Mzizi wa kitenzi (MZ)

Mzizi ni sehemu ya kitenzi isiyopunguzika au isiyobadilika ambayo haina viambishi vya namna yoyote, isipokuwa viambishi hupachikwa kabla au baada yake (Mdee, 2016). Fasili hii ya mzizi inalenga zaidi mizizi ya maneno ya lugha za Kibantu. Hii ni kwa sababu, lugha nyingi za Kibantu ni ambishi bainishi ambapo hubeba viambishi changamani vya namna mbalimbali ambavyo havichangamani na mzizi (Mgullu, 2012; Keet na Khumalo, 2017). Kwa hiyo, fasili hii haihusiani na mizizi ya vitenzi vya lugha zenye mofolojia ya kiruwaza kama Kiarabu na lugha nyingine za Kisemitiki (Djaffar, 2013). Mofolojia hii inatokana na tabia ya irabu za lugha za Kisemitiki kufumana na konsonanti zinazounda mizizi ya maneno ya lugha hizo. Pamoja na hayo, vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu havikutoholewa vikiwa na tabia hii.

Vilevile, Ud Deen (2005:47 - 48) amefafanua muundo wa mzizi wa vitenzi vya Kiswahili ambapo anasema kuwa muundo wa mzizi katika lugha ya Kiswahili na hata katika lugha nyingi za Kibantu ni silabi moja. Pia, anaeleza kuwa si mizizi yote ina muundo wa silabi moja, bali ipo ambayo ina silabi nyingi, hasa mizizi ya vitenzi vilivyokopwa katika lugha nyingine, hususani lugha ya Kiarabu. Pamoja na hayo, ufafanuzi huo unaotolewa hauoneshi namna uchanganuzi wa vitenzi hivyo unavyofanana na kutofautiana. Hata hivyo, muundo wa mzizi wa vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu umefafanuliwa kwa kina katika sehemu zinazofuata za makala hii; hivyo, maelezo ya Ud Deen (2005) yamethibitika zaidi.

Mbali na hayo, Hurskainen (1992) anauelezea mzizi wa kitenzi cha Kibantu kwamba unakuwa katikati ya kitenzi, ambapo viambishi vya kauli za vitenzi mara nyingi hupachikwa baada yake. Kutokana na fasili hii ya Hurskainen, si lazima na si wakati wote kila mzizi wa kitenzi kuwa katikati. Kuna vitenzi ambacho vinaweza kuwa na viambishi kabla ya mzizi na kusiwe na viambishi baada yake na kinyume chake. Mzizi wa namna hii hatuwezi kusema uko katikati ya kitenzi. Kwa mfano, kitenzi *sahau* ambacho mzizi wake ni -sahau- ni kitenzi cha Kiswahili chenye asili ya Kiarabu ambapo kikiambikwa viambishi vya uambatizi kama vya kiima na njeo na kuwa *a-na-sahau* (*anasahau*) mzizi wake hautakuwa katikati bali utakuwa mwishoni. Kwa hiyo, mzizi unaokuwa katikati ya kitenzi ni ule wenye viambishi kabla (vya uambatizi) na baada yake (vya unyambuzi) kama katika kitenzi *wa-na-sahau-li-an-a* (*wanasahauliana*). Kwa ujumla, mzizi wa kitenzi ndio kiini cha kitenzi ambao viambishi vya namna mbalimbali hupachikwa kabla na/au baada yake.

Sambamba na hayo, mzizi hujitokeza katika nafasi ya saba katika ruwaza ya vitenzi vya lugha za Kibantu (rejea ruwaza ya Meeussen, 1967, kama alivyorejelewa na Nurse, 2008). Mzizi wa vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu nao huchukua nafasi hiyohiyo katika ruwaza hiyo (Hakimu, 2020). Inadhaniwa kuwa kitenzi kimoja kina mkururo wa nafasi mpaka kumi na moja (11) zenye viambishi vya ruwaza hiyo ambazo zimeegemezwa katika mzizi (Nurse, 2008). Hivyo, mzizi wa kitenzi unaweza kuwa ni sehemu ya neno isiyokuwa na irabu ya mwisho au shina ambayo hupachikwa viambishi mbalimbali. Katika vitenzi vya Kiswahili asilia na vile vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu, viambishi vinaambikwa kabla na baada ya mzizi.

Aina za mizizi na uhalisia wake

Mizizi ya vitenzi vya Kiswahili kwa ujumla (vile vya Kiswahili asilia na vyenye asili ya Kiarabu) imetofautiana kutokana na mazingira ya namna mbili: kwanza, kuna mazingira yanayoonesha vitenzi vyenye mizizi huru; pili, mazingira yanayoonesha vitenzi vyenye mizizi tegemezi. Kwa mujibu wa Mgullu (2012:104), mizizi huru ni ile inayoweza kusimama peke yake bila viambishi vyovyote na maana yake ikawa kamili. Kwa maana hii, mizizi huru inakuwa iko katika muundo wa shina. Shina ni mzizi wa neno ambao umeongezewa irabu ya mwisho (Mugaya, 2019). Kwa mazingira hayo ya shina, baadhi ya mashina ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu (kama *sahau* na *dharau*) yanakuwa ni mizizi huru kwa sababu yana irabu ya mwisho ambayo haiathiriwi na uambikaji wa viambishi mbalimbali. Pia, kuhusu mizizi tegemezi, Mgullu anaeleza kuwa ni ile ambayo katika matumizi halisi ni lazima iwekewe angalau kiambishi kimoja ndipo ilete maana inayoeleweka kwa sababu mizizi tegemezi ikiwa peke yake bila viambishi vya namna yoyote haileti maana.

Katika uhalisia, mizizi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu inatofautiana na mizizi ya vitenzi vya Kiswahili asilia kwa sababu mizizi ya vitenzi vya Kiswahili asilia ni tegemezi tu (Wesana-Chomi, 2013). Hii ina maana kuwa tofauti na vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu, vitenzi vya Kiswahili havina mizizi huru tukizingatia uchanganuzi wa wataalamu kama Ud Deen (2005), Kihore, Massamba, & Msanjila (2012), Mgullu (2012) na Wesana-Chomi (2013). Kwa hiyo, hali hii inadhirisha kuwa mizizi ya vitenzi vilivyokopwa kutoka katika Kiarabu vina mazingira tofauti vikilinganishwa na vile vya Kiswahili asilia.

Vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vilivyo na mizizi huru ni kama *dharau - dharaulia* na *sahau - sahaulia*. Kutokana na mifano hiyo inaonekana kwamba, kiambishi cha utendea {-li-} kimeambikwa kwenye mizizi *dharau* na *sahau*. Kiambishi {-li-} kimeambikwa baada ya mzizi kwa namna ulivyo bila kuathiri irabu ya mwisho ya kitenzi. Jedwali Na. 1 linaonesha mizizi huru ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu ambapo viambishi vimetenganishwa kwa kistari (-) kwa kuzingatia msingi wa Nadharia ya Mofolojia Leksika kwamba kila kiambishi lazima kioneshwe nafasi yake.

Jedwali Na. 1: Mizizi Huru katika Vitenzi vya Kiswahili vyenye Asili ya Kiarabu

Kitenzi	Utendea	Utendeka	Utendesha	Utendwa	Utendana
sahau	sahau-li-a	sahau-lik-a	sahau-lish-a	sahau-liw-a	sahau-li-an-a
dharau	dharau-li-a	dharau-lik-a	dharau-lish-a	dharau-liw-a	dharau-li-an-a

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Mifano katika jedwali Na. 1, inaonesha kuwa uchopekaji wa viambishi vya kauli za vitenzi (utendea {-li-}, utendeka {-lik-}, utendesha {-lish-}, utendwa {-liw-} na utendana {-an-} hauleti athari katika mzizi wa kitenzi

({sahau-} na {dharau-}). Hii inatokana na ukweli kwamba mizizi ni sehemu ya neno ambayo haibadilikibadiliki, haiongezeki wala haipunguzi viambishi (Mugaya, 2019).

Vilevile, vitenzi vya Kiswahili asilia na vile vyenye asili ya Kiarabu vina mizizi tegemezi. Mizizi tegemezi katika vitenzi hivyo inadhihirika kwa namna mbili: mizizi tegemezi ambayo iko wazi na ile ambayo haiko wazi. Mizizi ambayo iko wazi ni ile inayobainika kwa wepesi kutokana na mabadiliko yanayojitokeza baada ya uambikaji wa kiambishi chochote cha kauli ya kitenzi. Mizizi ambayo haiko wazi ina michakato ambayo irabu ya mwisho haibainiki kwa uwazi hata baada ya kuambika baadhi ya viambishi vya kauli za vitenzi (Hakimu, 2020). Vitenzi vya Kiswahili asilia na baadhi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vina mizizi tegemezi ambayo iko wazi. Tofauti inajitokeza katika mazingira ya mizizi ambayo haiko wazi katika baadhi ya vitenzi vyenye asili ya Kiarabu.

Kwa hali hiyo, vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vyenye mizizi tegemezi ambayo haiko wazi ni vile vinavyoishia na irabu {-e} na {-i} katika mashina yake. Jedwali Na. 2 linaonesha vitenzi vya Kiswahili vyenye mizizi ambayo haiko wazi kwa kuzingatia msingi wa Nadharia ya Mofolojia Leksika kwamba kila kiambishi lazima kioneshwe nafasi yake.

Jedwali Na. 2: Vitenzi vya Kiswahili vyenye Asili ya Kiarabu vyenye Mizizi ambayo Haiko Wazi

Kitenzi	Utendea	Utendeka	Utendesha	Utendwa	Utendana
rudi	rud-i-a	rud-ik-a	rud-ish-a	rud-iw-a	rud-i-an-a
badili	badil-i-a	badil-ik-a	badil-ish-a	badil-iw-a	badil-i-an-a
Fadhili	fadhil-i-a	fadhil-ik-a	fadhil-ish-a	fadhil-iw-a	fadhil-i-ana
Samehe	sameh-e-a	sameh-ek-a	sameh-esh-a	sameh-ew-a	sameh-e-an-a
Starehe	stareh-e-a	stareh-ek-a	stareh-esh-a	stareh-ew-a	stareh-e-an-a

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Jedwali Na. 2 linaonesha vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu ambavyo mizizi yake haiko wazi. Kutokana na jedwali hilo, inaonekana kuwa kiambishi cha utendeka kinaweza kuwa ni {-k-}/{-ik-}, utendwa ni {-w-}, utendewa ni {iw-} na utendesha ni {-sh-}/{-ish-}. Hivyo, iwapo tutasema viambishi vya kauli za vitenzi ziwe {-k-}, {-w-} au {-sh-}, basi mizizi ya vitenzi hivyo itaonekana kuwa ni huru kwa sababu vimeambikwa kwenye shina la kitenzi kama ilivyokuwa kwa *dharau* na *sahau*. Pia, iwapo tutasema viambishi viwe {-ik-}/{-ek-}, {-iw-}/{-ew-} na {-ish-}/{-esh-} kutokana na mwelekeo wa tangamano la irabu la mizizi hiyo, basi mizizi hiyo itakuwa sio huru bali ni tegemezi. Tangamano hilo la irabu limedhihirisha utokeaji wa mwingiliano kanuni za darajia za kifonolojia na kimofolojia. Hii inatokana na sababu kwamba uambikaji wa kiambishi cha kauli ya kitenzi kunategemeana na sauti maalumu iliyoko kwenye mzizi wa kitenzi hicho. Uwapo wa irabu /e/ katika mzizi -sameh- kwa mfano, umechangia mzizi huo kuweza kuambikwa kiambishi cha utendeka {-ek-} na kuwa *sameheka*. Kwa hiyo, kanuni ya mzunguko kamili ya Nadharia ya Mofolojia Leksika hudhihirika kwa sababu uambikaji wa viambishi vya unyambuzi na/au uambatizi katika darajia za kimofolojia unakuwa na matokeo yake katika darajia za kifonolojia (kama tangamano la irabu, udondoshaji wa sauti, mkazo nk.) na kinyume chake katika mazingira mengine.

Mbali na hayo, suala la mizizi hiyo katika Jedwali Na. 2 kuwa tegemezi linathibitishwa na mitazamo ya Polome (1967) na Wesana-Chomi (2013) kuhusu irabu hizo za mwisho za mizizi hiyo. Polome (1967:85) anaonesha kuwa, ikitokea kitenzi kikawa kinaishia na irabu ya mwisho (IM) {-e} au {-i}, kitenzi hicho kikiambikwa kiambishi cha kauli ya kitenzi kunatokea msinyao kwenye irabu hizo. Mifano anayoitoa Polome ni pamoja na *rudi - rudia* na *samehe - samehea*. Hii ina maana kwamba, viambishi vya utendea wa {-e-} na {-i-} vikiambikwa vinasinyaza irabu za mwisho katika vitenzi *rudi* na *samehe*. Vilevile, Wesana-Chomi (2013:64) anasema kuwa irabu ya mwisho ya mizizi kama *badili - badiliwa/badilika* na *tubu - tubiwa* humezwa na irabu ya kwanza ya kinyambulishi ({-iw-}/{-ik-}) yaani $i+i \rightarrow i$ na $u+i \rightarrow i$. Maelezo haya ya Polome na Wesana-Chomi yanaonesha kuwa viambishi vya kauli za vitenzi walivyotumia ni vile vinavyoonesha utegemezi wa mizizi hiyo. Hii inatokana na ukweli kwamba kitendo cha irabu za mizizi hiyo kuwa na mabadiliko ya kusinyazwa au kumezwa, kwa mujibu wa madai ya Polome na Wesana-Chomi, kinaonesha kuwa mizizi hiyo si huru bali ni tegemezi isiyo wazi.

Kama ilivyoielezwa awali, vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vina mizizi tegemezi ambayo iko wazi pia kama ilivyo katika vitenzi vya Kiswahili asilia. Mizizi hiyo inabainika katika vitenzi vinavyoishia na IM {-u} au {-a}. Katika vitenzi vinavyoishia na IM {-u}, uambikaji wa kiambishi chochote cha kauli ya kitenzi hufanya IM {-u}/{-a} kubainika kuwa si sehemu ya mzizi kwa uwazi. Jedwali Na. 3 linaonesha vitenzi vya Kiswahili asilia na vyenye asili ya Kiarabu vinavyoishia na irabu {-u} na {-a} ambavyo mizizi yake inabainika wazi.

Jedwali Na. 3: Vitenzi vya Kiswahili Asilia na vyenye Asili ya Kiarabu vyenye IM {-u-} na {-a} ambavyo Mizizi yake iko Wazi

Asili ya Kitenzi	Kitenzi	Utendea	Utendeka	Utendesha	Utendewa	Utendana
Kiarabu	Tubu	tub-i-a	tub-ik-a	tub-ish-a	tub-iw-a	tub-i-an-a
	Alifu	alif-i-a	alif-ik-a	alif-ish-a	alif-iw-a	alif-i-an-a
	Jibu	jib-i-a	jib-ik-a	jib-ish-a	jib-iw-a	jib-i-an-a
	Afua	afu-li-a	afu-lik-a	afu-lish-a	afu-liw-a	afu-li-an-a
	Rejea	reje-le-a	rej-ek-a	rej-esh-a	rej-ew-a	rej-e-an-a
Kiswahili asilia	Piga	pig-i-a	pig-ik-a	pig-ish-a	pig-iw-a	pig-an-a
	Sema	sem-e-a	sem-ek-a	sem-esh-a	sem-ew-a	sem-an-a
	Jenga	jeng-e-a	jeng-ek-a	jeng-esh-a	jeng-ew-a	jeng-an-a

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Kutokana na jedwali Na. 3, inaonekana kuwa kiambishi cha kauli yoyote ya kitenzi kikiambikwa, IM ya kitenzi {-u-} inapotea (yaani haionekani katika kitenzi). Mazingira ya upoteaji (udondoshaji) wa irabu /u/ kutokana na uambikaji wa kiambishi chochote cha kauli ya kitenzi unaonesha uathiriano baina ya kanuni za kimofolojia na kifonolojia. Kwa hiyo, udondoshaji wa irabu hiyo unaonesha wazi mzizi wa kitenzi kuwa ni {-tub-} katika kitenzi *tubu*, {-alif-} katika kitenzi *alifu* na {-jib-} katika kitenzi *jibu*. Pia, kama ilivyobainika kwenye vitenzi vinavyoishia na IM {-e-} na {-i-}, utendana {-an-} pia unaonekana kama umechopekwa kwenye mizizi huru au umeambatana na kiambishi cha utendea {-i-}. Msimamo uliochukuliwa katika makala hii ni kwamba utendea wa {-i-} umeambatana na utendana wa {-an-} kama inavyoonekana katika jedwali Na. 3. Pamoja na hayo, mizizi ya vitenzi vya Kiswahili asilia na vile vyenye asili ya Kiarabu vinavyoishia na IM {-a} inaonekana kuwa iko wazi. Hii ni kwa sababu uambikaji wa viambishi vya kauli za vitenzi hauathiri IM {-a}. Hivyo, inabainika wazi kuwa kiambishi cha kauli ya kitenzi kimechopekwa baina ya mzizi na IM {-a}.

Miundo ya mizizi ya vitenzi

Miundo ya mizizi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu na vile vya Kiswahili asilia imebainishwa kwa kuzingatia muunganiko wa konsonanti na irabu zinazounda mzizi husika. Muunganiko huu umesaidia kubaini ufanano na utofauti wa mzizi wa vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu na vile vya Kiswahili asilia. Hili limejengwa katika msingi kwamba, muundo wa mzizi katika baadhi ya lugha za Kibantu huwa KIK (Konsonanti-Irabu-Konsonanti) na nyingine huwa na KI (Konsonanti-Irabu), chache huwa na muundo mrefu wa mzizi (KI-IK au KIK-KI) kutokana na upoteaji wa konsonanti ya mwisho au ya pili kutoka mwisho (Nurse & Philippson, 2003; Nurse, 2008). Kwa hiyo, sehemu hii inaonesha miundo ya mizizi ya vitenzi hivyo kwa kuanza na vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu ambavyo vina miundo ifuatayo ya mizizi kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

Jedwali Na. 4: Miundo ya Mizizi ya Vitenzi vya Kiswahili vyenye Asili ya Kiarabu

KIK	IKIK	KIKI	IKI	KI	IK	KIKII
taw-a	abud-u	raju-a	aki-a	dhi-i	udh-i	dharau
rud-i	alif-u	nuku-u	afu-a			sahau
sif-u	daraj-i	kina-i				

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Pamoja na miundo hiyo ya mizizi ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu katika jedwali Na. 4, miundo ya mizizi ya vitenzi vya Kiswahili asilia ina mazingira yanayofanana na hiyo (ya vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu) na kutofautiana nayo. Hivyo, Jedwali Na. 5 linaonesha muundo wa mizizi ya vitenzi vya Kiswahili asilia.

Jedwali Na. 5: Miundo ya Mizizi ya Vitenzi vya Kiswahili Asilia

K	I	KIK	KIKI	KIKIK	KIK(N)KI	IKI	KI	IK	IKIK
l-a	u-a	lim-a	paku-a	pelek-a	tambe-a	oko-a	za-a	og-a	ogop-a
p-a	o-a	som-a	koso-a		kimbi-a	opo-a	zo-a	on-a	okot-a
f-a		lip-a	binu-a		tanguli-a	umi-a	po-a	uz-a	uliz-a
ny-a		pat-a			ondo-a		lo-a	ib-a	

Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Kutokana na Jedwali Na. 4 na 5, K inamaanisha (Konsonanti), I (irabu), KIK (Konsonanti-Irabu-Konsonanti), KIKI (Kinsonanti-Irabu-Konsonanti-Irabu), IKI (Irabu-Konsonanti-Irabu), KI (Konsonanti-Irabu), IK (Irabu-Konsonanti-Konsonanti) na KIKII (Konsonanti-Irabu-Konsonanti-Irabu-Irabu), KIKIK (Konsonanti-Irabu-Konsonanti-Irabu-Konsonanti) na KIK(N)KI (Konsonanti-Irabu-Konsonanti (Nazali)-Konsonanti-Irabu).

Majedwali hayo (4 na 5) yanaonesha kuwa mizizi ya vitenzi vya Kiswahili asilia na ile ya vyenye asili ya Kiarabu inafanana katika muundo wa KIK, KIKI, IKI, KI na IK. Hii inadhihirisha kuwa vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vimefuata mkondo wa Kiswahili/Kibantu katika usarufishaji wake tofauti na asili ya mizizi yake ya mofolojia ya kiruwaza ilivyo. Hata hivyo, kuna tofauti ya miundo ya mizizi katika vitenzi hivyo. Miundo K, I, KIKIK na KIK(N)KI ya vitenzi vya Kiswahili asilia haikudhihirika katika vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu kwa mujibu wa data iliyoshughulikiwa. Vilevile, muundo wa KIKII unajitokeza katika vitenzi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu na si katika vitenzi vya Kiswahili asilia. Hali hii inaonesha kuwa vitenzi hivyo havijasarufishwa kikamilifu kama muundo wa vitenzi vya Kiswahili asilia katika vitenzi vyote.

Kwa ujumla, mizizi ya vitenzi hivyo (baadhi ya vitenzi vyenye asili ya Kiarabu na vya Kiswahili asilia) ina miundo ya mizizi sawa na mizizi ya

vitenzi vingine vya Kibantu. Muundo wa mzizi katika baadhi ya lugha za Kibantu huwa KIK (Konsonanti-Irabu-Konsonanti) na nyingine huwa na KI (Konsonanti-Irabu), chache huwa na muundo mrefu wa mzizi (KI-IK au KIK-KI) kutokana na upoteaji wa konsonanti ya mwisho au ya pili kutoka mwisho (Nurse & Philippon, 2003; Nurse, 2008). Vitenzi vingi vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu vina miundo ya mizizi ya KIK, IKIK na KIKI. Hii inatokana na ukweli kuwa mizizi ya vitenzi vingi inaishia na konsonanti na michache huishia na irabu. Kwa hiyo, kila kitenzi cha Kiswahili chenye asili ya Kiarabu kina nafasi ya mzizi (huru au tegemezi) ambayo viambishi mbalimbali huambikwa kabla au baada yake. Pia, kila kitenzi cha Kiswahili asilia kina mzizi tegemezi kwa mujibu wa data ya makala hii.

Hitimisho

Makala hii imeshughulikia mizizi ya vitenzi vya Kiswahili asilia na ile ya vitenzi vyenye asili ya Kiarabu. Vitenzi hivyo vimeshughulikiwa kwa kuzingatia michakato inayoibadili na isiyobadili mizizi hiyo. Hii ina maana kwamba, iwapo mzizi umeonekana kubadilika kwa mchakato wowote (kama kusinyazwa, kumezwa, kupotea au kusogea kwa irabu ya mwisho ya kitenzi), mzizi huo umechukuliwa kuwa mzizi tegemezi katika vitenzi vya Kiswahili. Vilevile, iwapo uambikaji wa viambishi vyovyote haubadili hali ya shina la kitenzi, basi shina hilo limechukuliwa kama mzizi huru wa kitenzi. Kutokana na ufafanuzi huo, vitenzi vya Kiswahili vyenye asilia ya Kiarabu vina mizizi huru na tegemezi wakati vitenzi vya Kiswahili asilia mizizi yake ni tegemezi tu. Kwa hiyo, kutokana na ubainishaji wa mipaka ya viambishi, mabadiliko ya baadhi ya sauti baada ya uambikaji wa kiambishi cha kauli ya kitenzi na ufafanuzi linganishi wa mizizi ya vitenzi

vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu na vile vya Kiswahili asilia, muundo wa mzizi wa vitenzi vya Kiswahili umethibitika katika makala hii.

Marejeleo

BAKITA. (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Limited.

Buberwa, A. (2015). *Mofolojia ya Majina ya Mahali ya Kiswahili na Kihaya katika Jamii ya Wahaya: Uzingativu wa Masuala ya Kiisimujamii*, (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Djaffar, F. (2013). *Morphological Derivations and Inflections in an Algerian Arabic Dialect*, (Unpublished M.A Thesis), The University of Malaisia, studentsrepo.um.edu.my/5416/1/MORPHOLOGICAL_DERIVATIONS.pdf%0D.

Gichuru, T.M. (2010). *Uchanganuzi wa Nomino Ambatani za Kiswahili: Mtazamo wa Mofolojia Leksia*, (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. ir-library.ku.ac.ke.

Hakimu, J. (2020). *Ubantuishaji wa Kimofolojia katika Vitenzi vya Kiswahili vyenye Asili ya Kiarabu*, (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hurskainen, A. (1992). Disambiguation of Morphological Analysis in Bantu Languages. *Proceedings of the 16th Conference on Computational Linguistics, Volume 1*, 568 - 573. <https://doi.org/10.3115/992628.992726>.

Katamba, F. (1993). *Morphology*. New York: St. Martin's Press.

Keet, C.M. & Khumalo, L. (2017). Grammar Rules for the isiZulu Complex Verb. *Southern African Linguistics and Applied Language Studies*, 35(2), 183 - 200. <https://doi.org/10.2989/16073614.2017.1358097>.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B. & Msanjila, Y.P. (2012). *Sarufi Maumbo*

ya *Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuho*. Dar es Salaam: TUKI.

Kiparsky, P. (1982). Lexical Phonology and Morphology. *Encyclopedia of Language & Linguistics*, 94 - 97. <https://doi.org/10.1016/b0-08-044854-2/00088-2>.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mdee, J. (2016). Patterns of Swahili Verbal Derivatives: An Analysis of their Formation. *Huria: Journal of the Open University of Tanzania*, 21(1), 43 –51.

Mgullu, R.S. (2012). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Mugaya, T.S. (2019). *Mofolojia Changamani ya Kiswahili*. Dodoma: FEX Connect Publishers.

Nurse, D. & Philippson, G. (2003). *The Bantu Languages*. USA: Taylor & Francis Routledge.

Nurse, D. (2008). *Tense and Aspect in Bantu*. USA: Oxford University Press.

Polome, E.C. (1967). *Swahili Language Handbook*. USA: Center for Applied Linguistics.

Ud Deen, K. (2005). *The Acquisition of Swahili*. Amsterdam: John Benjamin Publishing Company.

Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TATAKI.